# TAARIFA YA WAJUMBE WA TANO WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR WANAOWAKILISHA KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUHUSU NAMNA WALIVYOWAKILISHA BARAZA KATIKA BUNGE

## 0.1 UTANGULIZI

***Historia ya Uwakilishi wa Wajumbe wa Baraza katika Bunge la Jamhuri***

Baada ya kuasisiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964, pamoja na mambo mengine muhimu, liliundwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka huo 1964 lenye sura ya Muungano, likijumuisha Wajumbe wa Bunge kutoka bara na Zanzibar. Kuanzia kipindi hicho cha mwaka 1964 mpaka mwaka 1980 Wajumbe wa Bunge kutoka Zanzibar walikuwa hawachaguliwi kupitia majimbo ya uchaguzi kama yalivyo hivi sasa. Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi ambalo kwa wakati huo vile vile ilikuwa ndiyo chombo cha kutunga Sheria kwa Zanzibar walikuwa ndiyo Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Wakati huo Baraza la Mapinduzi lilikuwa na Wajumbe wapato 30 ambao ndiyo walikuwa Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Hivyo basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilishiriki moja kwa moja katika shughuli zote Bungeni na Maamuzi yote yaliyokuwa yakifanyika Bungeni Serikali ya Zanzibar ilishiriki moja kwa moja. Mwaka 1979 Zanzibar ilitunga Katiba yake ya kwanza ambayo pamoja na mambo mengine iliunda chombo cha kutunga sheria (Baraza la Wawakilishi).

Baraza la Wawakilishi liliundwa tarehe 12 Januari, 1980 na Mkutano wake wa kwanza wa kulizindua ulifanyika mnamo tarehe 14 Januari, 1980 katika Ukumbi wa Mnazimmoja ambao hivi sasa unajulikana kama Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakyl, ambaye alikuwa ndiye Spika wa mwanzo wa Baraza la Wawakilishi.

Baraza hilo la Wawakilishi lilijumuisha Wajumbe kutoka Baraza la Mapinduzi na Wajumbe wengine ambao waliteuliwa na Rais na wengine waliochaguliwa kutoka katika Jumuiya mbali mbali za Chama na Kamati za Mapinduzi za Wilaya na Mikoa.

Kufuatia mabadiliko hayo, mnamo tarehe 2 Januari, 1980, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 (Sheria namba 1 ya 1980) ambayo yaliweka masharti mapya yalitokana na kutungwa kwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979.

Miongoni mwa masharti hayo ni kuweka utaratibu wa kuchagua wabunge kutoka Zanzibar ambapo Baraza la Wawakilishi lilipewa uwezo kuchagua Wajumbe wasiozidi 32 kutoka miongoni mwa Wajumbe wake na kutoka nje ya Baraza hilo. Marekebisho hayo yaliendeleza ushiriki wa moja kwa moja wa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kuwa Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa idadi iliyoainishwa katika Sheria hiyo. Mnamo tarehe 9 Oktoba, 1984, Baraza la Wawakilishi Zanzibar lilipitisha azimio la kutunga Katiba mpya ambayo ilifuta Katiba ya mwaka 1979.

Sambamba na hatua hiyo, tarehe 30 Oktoba, 1984 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya Marekebisho ya Tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 (sheria namba 15/1984) ambayo ilifanya marekebisho makubwa katika Katiba hiyo, moja wapo ni Muundo na aina za Wabunge wa Bunge la Jamhuri.

Kifungu cha 13 cha Sheria hiyo kilichorekebisha ibara ya 66 ya Katiba, kiliweka idadi ya Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilshi watakaochaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wake.

Mabadiliko hayo yalipunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliokuwa wakiingia Bungeni kutoka 32 na kubakisha watano ili kuendeleza na kudumisha muunganiko chanya wa vyombo hivi viwili (Baraza na Bunge) ulioanzishwa na waasisi wa Muungano wetu. Utaratibu huu umebakia tokea kuasisiwa kwa Bunge mpaka hivi sasa. Vilevile utaratibu huo unaendelea kukumbusha kizazi cha sasa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeasisiwa na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi ambalo kwa wakati huo pia lilikuwa ni Baraza la Kutunga Sheria za Zanzibar na baaadaye Baraza la Wawakilishi.

***Wajumbe wa Baraza waliowahi kuliwakilisha Baraza Bungeni tokea mwaka 1985 mpaka sasa.***

Tokea mwezi Januari, 1985, baada ya Zanzibar kuanza kutumia Katiba mpya, katika awamu mbalimbali kumekuwa na Wajumbe Wawakilishi waliochaguliwa kuliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ambao ni kama ifuatavyo:-

**Mwaka 1985-1990,** *alikuwa:-*

1 Mheshimiwa Maulid Makame Abdullah
2 Mheshimiwa Salmin Amour Juma
3 Mheshimiwa Abdallah Said Haji
4 Mheshimiwa Soud Yussuf Mgeni* *Mhe. Abdulla Rashid Abdulla*
5 Mheshimiwa Ramadhan Abdalla Shaaban

**Mwaka 1990-1995,** *alikuwa:*

1. Mheshimiwa Amani Abeid Karume
2. Mheshimiwa Amina Salum Ali
3. Mheshimiwa Abdulla Rashid Abdulla
4. Mheshimiwa Mohammed Abdulla Khamis
5. Mheshimiwa Khamis Suleiman Dadi

**Mwaka 1995-2000,** *alikuwa:*

1. Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna
2. Mheshimiwa Amina Salum Ali
3. Mheshimiwa Idd Pandu Hassan
4. Mheshimiwa Mussa Ame Silima
5. Mheshimiwa Mwalimu Haji Ameir

**Mwaka 2000-2005,** *alikuwa:*

1. Mheshimiwa Ramadhan Nyonje Pandu
2. Mheshimiwa Mohammed Aboud Mohammed
3. Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid
4. Mheshimiwa Khamis Salum Abdulla
5. Mheshimiwa Shariffa Mbarouk Khamis

**Mwaka 2005-2010,** *alikuwa:*

1. Mheshimiwa Ali Haji Ali

2. Mheshimiwa Harun Ali Suleiman
3. Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim
4. Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakar
5. Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Ferej

**Mwaka 2010-2015,** *alikuwa:*

1. Mheshimiwa Mussa Khamis Silima **Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa*
2. Mheshimiwa Shawana Bukheit Hassan
3. Mheshimiwa Asaa Othman Hamad
4. Mheshimiwa Zahra Ali Hamad; na
5. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub

**Mwaka 2015-2020,** *alikuwa:*

1. Mheshimiwa Machano Othman Said
2. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub
3. Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir
4. Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu
5. Mheshimiwa Amina Idd Mabrouk

**Mwaka 2020-2025,** *wanawakilisha:*

1. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis
2. Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo
3. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar
4. Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman
5. Mheshimiwa Ameir Abdulla Ameir

Miongoni mwa Wajumbe waliotajwa hapo juu ambao waliwahi kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliowakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wamewahi baadaye kuwa katika nyadhifa kubwa katika mihimili mengine ya nchi kama vile Rais na Spika na miongoni mwao ni wewe Mheshimiwa Spika wetu Zubeir Ali Maulid. Hata hivyo, wapo ambao tayari wameshatangulia mbele ya haki na namuomba Mwenyezimungu awasamehe makosa yao na azilaze roho zao mahali pema peponi. Amin.

Wajumbe wa Bunge waliochaguliwa na Baraza kuanzia mwaka 2020 wanaendelea kuliwakilisha Baraza la Wawakilishi Bungeni. Aidha hawa ndiyo Wajumbe wa mwanzo, baada ya kipindi kirefu, kutekeleza Kanuni ya 137 (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza inayowataka kuwasilisha Barazani taarifa ya namna ya uwakilishi wao Bungeni.

***Msingi wa Kisheria wa Wajumbe wa Baraza kuwepo Bungeni***

Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi wanaowakilisha Bungeni wapo kwa mujibu wa kifungu cha 66 (1) (c ) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Wajumbe hao wanachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

***Utaratibu wa Kupatikana Wajumbe wa Baraza katika Bunge***

Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020 zimeweka utaratibu wa kupatikana Wajumbe watano watakaowakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kanuni ya 137 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zimetaja masharti ya kupatikana kwa Wajumbe hao. Kanuni hiyo inaeleza kuwa:-

> *"kila chama chenye Wajumbe katika Baraza la Wawakilishi kitakuwa na haki ya kupata Mbunge mmoja kwa kila viti kumi ambavyo chama husika kimepata miongoni mwa Wajumbe wa Kuchaguliwa kwenye Majimbo. Isipokuwa kwamba, chama chenye haki ya kupata Wabunge wawili au zaidi basi angalau nafasi moja itakuwa ya Mjumbe mwanamke".*

Utaratibu wa uchaguzi wa Wajumbe hao ni kwa njia ya kura za siri ambapo kila Chama kinawasilisha majina ya wagombea wa nafasi hizo kwa mujibu viti inavyostahiki. Kila chama kinakuwa na utaratibu wake wa ndani wa kupata majina ya wagombea wa nafasi hizo. Wajumbe wa Baraza wanapata nafasi ya kuwapigia kura Wajumbe ambao majina yao yamewasilishwa na vyama au chama chao kugombea.

## 0.2 MAJUKUMU YA WABUNGE WATANO

Wabunge hao mara wanapochaguliwa kwenye Baraza wanatakiwa kuapishwa Bungeni kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni zinazoendesha Bunge kwa kuwa wanakuwa na sifa kamili za kuwa

Wajumbe wa Bunge. Kazi na majukumu yao ni zile zile zilizowekwa katika ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo ni:-

- Kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya Umma.
- Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti.
- Kujadili na kuridhia Mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo.
- Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo Sheria.
- Kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Wajibu huo wa Kikatiba unawahusu pia Wajumbe wa Bunge watano wanaowakilisha Baraza Bungeni.

**Uwakilishi wa Wabunge Watano wa Baraza wakiwa Bungeni**

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi Wajumbe watano wanaowakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri wametoka mbali tokea wakati Baraza hili likiwa sehemu ya Baraza la Mapinduzi lililokuwa na wajumbe waliokuwa wakishiriki moja kwa moja Bungeni wakiwa Wajumbe wa Bunge hilo.

Ushiriki huo umeendelea kuwepo kwenye Katiba ingawa idadi ya Wajumbe imepungua kutoka Wajumbe 32 hadi kufikia Wajumbe watano baada ya mabadiliko kadhaa ya katiba zote mbili.

Hata hivyo, Kanuni za Baraza haziweki wazi namna ya Uwakilishi wa Wabunge hao wakiwa Bungeni kuliwakilisha Baraza, badala yake Kanuni ya 137 (5), imelipa uwezo Baraza la Wawakilishi kutoa azimio mahususi kwa Wajumbe hao watano, ili liweze kutekelezwa kwa niaba ya Baraza. Maana yake ni kuwa Baraza linaweza kutoa azimio lenye maelekezo mahususi kwa wajumbe hao na kuyawasilisha Bungeni.

***Wajumbe Wa Baraza Bungeni kuleta Taarifa Barazani***

Kanuni ya 137 (6) imeweka masharti kwa Wajumbe wa Baraza wanaowakilisha Bungeni kumchagua Mjumbe mmoja miongoni mwao

kuwasilisha taarifa Barazani itakayoeleza namna walivyowakilisha Baraza la Wawakilishi wakiwa Bungeni. Utaratibu huo wa Kikanuni kwa kipindi kirefu umekuwa hautekelezwi ingawa Baraza limekuwa likichagua Wajumbe hao kila awamu. Hivyo basi, taarifa hii itakuwa ni ya mwanzo kutekeleza masharti ya Kanuni ya 137 (6) baada ya miaka mingi kupita.

Sambamba na hilo, na kwa bahati mbaya taarifa hii inawasilishwa kukiwa hakuna azimio lililowahi kutolewa na Baraza na kupatiwa Wajumbe wanaowakilisha Bungeni na kuleta mrejesho. Hivyo basi, taarifa hii itajielekeza kwenye mambo mbalimbali ya msingi ambayo Wajumbe waliyafanyia kazi wakiwa Bungeni kwa maslahi wa Wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

## 0.3 MAENEO YALIYOFANYIWA KAZI

Wajumbe watano wa Baraza walishiriki katika shughuli mbali mbali za Bunge kwa mujibu wa Kanuni. Njia mbali mbali zimetumika kwa Wajumbe kufanyakazi ya uwakilishi Bungeni kama vile:- kupitia Kamati za Kudumu za Bunge, Vipidi vya Maswali na Majibu, vikao vya Kutunga Sheria, vikao vya kujadili Bajeti, vikao vya kujadili taarifa mbali mbali za Mipango ya Serikali, mijadala ya ripoti za Kamati na majadiliano ya kuidhinisha mikataba mbali mbali ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inaingia.

## 0.4 MASUALA YALIZOWASILISHWA BUNGENI NA MREJESHO WAKE

Kupitia maeneo hayo yaliyofanyiwa kazi, hoja mbali mbali ziliwasilishwa na kupatiwa mrejesho wake kama ifuatavyo:-

***i. Kuimarisha na Kudumisha Muungano***

Miongoni mwa michango iliyowasilishwa na Wajumbe wa Baraza wanaowakilisha Bungeni ni maoni, ushauri na mapendezo yatakaosaidia kudumishwa na kuimarishwa Muungano kwa kusimamia na kutiliwa mkazo maeneo yafuatayo:-

a. Wananchi kuendelea kuelimishwa umuhimu na faida za Muungano kwa nchi zote mbili. Wajumbe wamepongeza hatua nzuri ya Serikali zote mbili kukutana mnamo tarehe 17/10/2020 kutiliana saini

kuziondoa hoja tano za Muungano kama vile ushirikishwaji wa Serikali ya Zanzibar kwenye masuala ya Kimataifa na kikanda, ushiriki wa Zanzibar kwenye masuala ya Afrika Mashariki lakini pia uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Hatua hii ni nzuri na kupongezwa kwa Serikali zote mbili.

b. Kwa kuwa utatuzi wa changamoto za Muungano unakwenda vizuri kupitia vikao vya pande zote mbili, wananchi wapatiwe taarifa kufahamishwa ni changamoto gani zimeshatatuliwa na utekelezaji wake unaanza wakati gani na unaendelea vipi. Maelezo ya ufafanuzi wa Serikali kuhusu maoni haya ni kuwa utatuzi wa changamoto utaendelea na wananchi watapatiwa taarifa pamoja na kuendelea kupatiwa elimu na uwelewa kuhusu faida za Muungano.

c. Viongozi (Mawaziri) wafatilie utekelezaji wa changamoto zilizotatuliwa kwa kuwa viongozi wa ngazi za juu ndiyo wanaokubaliana lakini baadhi ya watendaji wa ngazi za chini wanakuwa wazito kutekeleza mambo yaliyokubaliwa kutatuliwa. Kwa mfano, changamoto ya gharama za mizigo inayosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam na usafirishaji wa gari kutoka upande mmoja kwenda mwengine tayari zimeshapatiwa ufumbuzi lakini utekelezaji wake unahitaji kufatiliwa kwa watendaji wa ngazi za chini kuhakikisha wanatekeleza. Maoni haya Serikali imeyachukuwa na kufanyiwa kazi.

d. Ucheleweshaji wa kuweka saini mikataba ya Kimataifa ambayo inahusu Zanzibar kama vile ujenzi na ukarabati wa Hospitai ya Mnazimmoja, unaotokana na mkataba wa ufadhili wa **"Saudi Fund"** pamoja na na ujenzi wa barabara ya Chake Chake-Wete. Maelezo ya majibu kutoka na mchango huo ni kuwa miradi hiyo tayari uwekaji saini umeshakamilika na ipo miradi mengine ambayo inasuburi itakamilishwa pia.

e. Katika kudumisha Muungano moja wapo ni kuenzi na kuthamini mchango wa viongozi wa Muungano wetu. Ilielezwa kuwa hali ya kijiji anachotoka Marehemu Dokta Omar Ali Juma *(aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano)* siyo nzuri, mfano miundombinu

chakavu ya barabara inayoelekea eneo alilozikwa na eneo ambalo limejengwa skuli iliyopewa jina lake. Barabara hiyo hali yake ni chakavu na inaunganisha barabara kuu. Maelezo ya majibu ya maoni haya ni kuwa Serikali imechukuwa mchango huo wa Mbunge na itaufanyia kazi ili kuenzi na kuthamini kazi ya kiongozi huyo.

f. Kuimarishwa Stahiki za Wafanyakazi katika Taasisi za Muungano (Jeshi la Polisi). Wajumbe wa Baraza walishauri Serikali kufuatilia stahiki za askari Polisi ambao wanatakiwa wapatiwe asilimia 15% ya mishahara yao kama malipo ya pango (rent), badala yake fedha hizo wanapatiwa pungufu. Serikali imeshauriwa kuitatuwa changamoto hiyo kwa mujibu wa taratibu, ushauri ambao umechukuliwa na Serikali kufanyiwa kazi.

g. Kufungwa kwa vituo vidogo ya Polisi vya Kidongo chekundu, Jang'ombe na Beit el Ras kinyume na makusudio yaliyowekwa. Maelezo ya majibu ya suala hili kutoka Serikalini ni kuwa vituo kituo kidogo cha Polisi cha Kidongochekundu kilijengwa mwaka 1993, kituo kidogo cha Polisi cha Jang'ombe kilijengwa mwaka 2002 na kile cha Beit el Ras kimejengwa mwaka 1994. Mwaka 2019 vituo hivyo vilifungwa kutokana na upungufu wa askari Polisi. Hata hivyo, kituo kidogo cha Polisi cha Jang'ombe tayari kimeshafunguliwa na vituo vyengine vilivyobaki vitafunguliwa baada ya kupatikana askari wa kutosha kutoka chuo cha Polisi Moshi. Aidha, vituo ambavyo vimechakaa kutokana na kufungwa muda mrefu, Serikali imeagiza Kamisheni ya Polisi Zanzibar kuvifanyia ukarabati kabla ya kupelekwa askari watakaomaliza mafunzo kutoka Chuoni. Mpaka taarifa hii inawasilishwa tayari Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ameshalitekeleza kwa kutembelea vituo hivyo na kutoa maelekezo.

h. Kuendelezwa mashirikiano baina ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zile za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kubadilishana uzoefu wa mambo mbali mbali ambayo upande mmoja yapo na upande mwengine hakuna mfano Wizara zinazosimamia

sekta ya utalii n.k. Maelezo ya majibu ya maoni haya ni kuwa mashirikiano hayo yapo na yataendelea kuimarishwa kila siku.

***ii. Kuimarishwa masuala ya Uchumi, mapato na Biashara***

Katika eneo hili Wajumbe wa Baraza Bungeni walishauri na kutoa mapendekezo yao katika maeneo yafuatayo:-

a. Kuwekwa mazingira rafiki kwa wawekezaji kuweza kujenga uchumi shindani na viwanda kwa kupunguza viwango vikubwa vya riba, kuondoa urasimu kwa kuweka kituo kimoja cha huduma kwa wawekezaji (one stop center) na kuwekeza kwenye kilimo kwa kuwaelimisha vijana namna ya kuzalisha malighafi za kilimo kwa ajili ya viwanda. Mapendekezo hayo yamechukuliwa kuwa sehemu ya mikakati ya kuimarisha uwekezaji nchini.
b. Ufafanuzi wa kodi ya PAYEE inayolipwa na Wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanyakazi upande wa Zanzibar. Wajumbe walitaka kujua kodi hiyo kutoongezeka katika mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ilikuwa bilioni 21 kama mwaka uliotangulia kwa vile mapato hayo yanakwenda moja kwa moja kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Maelezo ya majibu ya Serikali ni kuwa suala hili linakwenda kwa taratibu zilizowekwa baina ya pande zote mbili.
c. Serikali ya Jamhuri ya Muungano imeshauriwa kuendeleza suala la uchumi wa buluu kwa upande wa Zanzibar. Kwakuwa kuna mpango wa kununua meli nne za uvuvi katika bahari kuu ni vyema fedha za ndani zikatengwa ili kukamilisha mipango hiyo badala ya kutegemea wafadhili. Maoni haya yamepokelewa na ahadi imetolewa kuwa yatafanyiwa kazi.
d. Serikali imeshauriwa kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu tozo za miamala ya simu na kama makusanyo ya fedha hizo yatapatikana kwa Zanzibar. Maelezo ya majibu ya ushauri huo ni kwamba tozo hizo zinalenga kuimarisha huduma za jamii kwa wananchi wote wa

Tanzania ikiwemo Zanzibar, hivyo makusanyo ya tozo hizo pia yatapelekwa Zanzibar.

e. Changamoto ya Malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hayana uhalisia. Inaonekana kuwa pamoja na kuwepo mifumo ya ukusanyaji ya kisasa bado kuna uvujaji wa mapato mfano katika mfumo wa ITAX ambao unakusanya kodi kwa walipa kodi wadogo mapato mengi yanapotea. Katika mfumo wa *CIMIS* ambao unahusu ushughulikiaji wa mashauri ya walipa kodi unaonekana na mapungufu kwa vile ulikusudiwa kupunguza wingi wa mashauri ambayo bado hayajapungua. Mwaka 2018 mashauri yalikuwa 770 lakini kufikia mwaka 2020 baada ya mfumo kuwepo yameongezeka kuwa 1097. Mashauri hayo yana jumla ya fedha za kodi zaidi ya trilioni 360. Majibu ya hoja hii yatatolewa katika Mkutano wa Bunge wa mwezi wa Septemba.

***iii.Masuala ya Kisheria (Marekebisho ya Sheria za Fedha, Kodi na Usimamizi wa Fedha)***

Katika eneo hili Wajumbe wa Baraza Bungeni waliwasilisha maoni na mapendekezo yao kama ifuatavyo:-

a. Marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye bidhaa zinazosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania bara na kutoka Tanzania bara kwenda Zanzibar ni hatua nzuri ambayo inahitaji ufuatiliaji katika kuitekeleza. Serikali imeshauriwa kuwa isiishie kwenye kufanya marekebisho peke yake lakini pia kuwepo na ufatiliaji. Maoni hayo yamechukuliwa kufanyiwa kazi ili kuleta ufanisi wa utekelezaji.

b. Katika marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasabu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021 ambayo yametaja kuwa Taasisi zenye marejesho ya faida kuanzia Tsh. Milioni 500 mpaka milioni 700 ziajiri Wahasibu wenye vyeti vya ithibati ya Uhasibu (CPA). Katika marekebisho hayo Wajumbe wa Baraza wamependekeza kuwa kwenye Bodi za Mashirika ya Umma

awepo Mjumbe wa Bodi mwenye taaluma ya kihabu angalau mmoja kusaidia kutoa miongozo ya kitaalamu. Pendekezo zuri na litanzingatiwa katika marekebisho ya sheria.

c. Sheria ya Bodi ya Uhasibu (NBAA) inahusu upande wa Tanzania bara na kwa upande wa Zanzibar kuna hatua za kuanzisha Bodi yake Uhasibu na Wakaguzi wa Hesabu kama hiyo ya Tanzania bara. Wajumbe wa Baraza Bungeni walionesha wasiwasi wao juu ya utambuzi wa Wahasibu na Wakaguzi watakaosajiliwa na Bodi itakayoanzishwa Zanzibar wataweza kufanya kazi Tanzania bara. Na kuhusu uwakilishi wa Bodi hizi katika Taasisi za Kimataifa ambapo NBAA tayari ni mwanachama wa Bodi za kimataifa kama vile *International Federation of Accountants* (IFAC), *Pan Africa Federation of Accountants* (PAFA), *International Organization of Supreme Audit Institutions* (INTOSAI) na *African Organizations of Supreme Audit Institutions* (AFROSAI), ni vipi Zanzibar itakapoanzisha Bodi yake itaweza kujiunga na taasisi hizo ili kuondoa ukakasi kama ilivyo kwa baadhi ya Taasisi nyengine zinazofanana na hizo kama vile ZFF na TFF. Maelezo ya majibu yalikuwa suala hilo litawekewa utaratibu mzuri wa uendeshaji kwa pande zote mbili.

d. Ushirikishwaji wa Wadau mbali mbali katika kutekeleza Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Sheria namba 2 ya mwaka 2019. Wajumbe wa Baraza katika Bunge walihoji ni kwa namna gani wadau hao wanashirikishwa katika utekelezaji wa Sheria hiyo. Wadau hao ni kama vile Shirika la Bandari, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege n.k Vilevile, Wajumbe walishauri Serikalli kutunga Kanuni za Sheria hiyo ili kurahisisha utekelezaji wake kwa kuwa tokea ilipotungwa Sheria hiyo haijawekewa Kanuni zake. Maelezo ya majibu ya pendekezo hilo ni kuwa mpango wa kuweka Kanuni za Sheria hiyo unaendelea na karibuni Kanuni hizo zitakuwa tayari.

***iv. Ushirikishwaji wa Viongozi katika Mradi wa TASAF III***

Katika eneo hili Wabunge wa Baraza walishauri na kutoa mapendekezo yao kama ifuatavyo:-

a. Imeonekana katika taarifa ya Serikali kuwa Zanzibar imefanya vizuri katika utekelezaji wa Miradi ya TASAF, hivyo Wajumbe walishauri kuwa katika awamu ya tatu ya mradi TASAF ushirikishwaji wa viongozi uendelezwe katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Majimbo. Katika awamu ya pili ushirikishwaji ulikuwa mzuri katika ngazi hizo, hivyo mradi uendelee kutoa mashirikiano hayo katika awamu ya tatu ya mradi. Ushauri huo umepokelewa na utekelezaji wake utafuata na tayari Waziri husika ameshafanya ziara mara mbili Zanzibar kuangalia utekelezaji wa baadhi ya miradi ya TASAF.
b. Wajumbe wamepongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Miradi ya TASAF ambayo matokeo ya utekelezaji yameonekana kwa vitendo. Pongezi hizo zimetokana na taarifa ya Serikali Bungeni kuonesha kuwa mradi wa TASAF umetekelezwa vizuri Zanzibar.

***v. Utatuzi wa Changamoto za Mazingira na Tabianchi***

Katika eneo hili muhimu Wajumbe wa Baraza Bungeni waliwasilisha maoni na mapendekezo yao kama ifuatavyo:-

a. Kuwekwe mikakati madhubuti ya uhifadhi wa mazingira kwa kuwa uharibifu wa mazingira unaleta athari katika sekta nyengine za kiuchumi kama vile utalii. Kwa kuwa Tanzania ina visiwa na sehemu za fukwe kumekuwa na athari za mmong'onyoko wa ardhi.
b. Athari ya kupanda kwa maji ya bahari, hatua zichukuliwe kudhibti hali hiyo mbaya, mfano eneo la Marumbi na maeneo mengine ya visiwa vya Zanzibar maji ya bahari yamepanda na kuleta athari kwenye maeneo wanayozikana watu. Maelezo ya majibu ya mapendekezo hayo ni kuwa Serikali kwa kutumia mifuko mitatu ya fedha za Mazingira watatenga fedha ya kukabiliana na hali hiyo

na tayari yapo maeneo hatua zimeanza kuchukuliwa kama vile Dar es Salaam na Tanga na maeneo mengine yatafuatia.

***vi. Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kupatikana kwa Wakati***

Katika eneo hili Wajumbe walishauri Serikaili kuhakikisha wanafunzi wanaomba mikopo ya Elimu ya Juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania kuhakikisha mikopo inapatikana kwa wakati ili wanafunzi wasihangaike. Maelezo ya majibu ya ushauri huo ni kwamba Serikali imeweka fedha na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu itahakikisha wanafunzi wanapatiwa fedha zao kwa wakati bila ya usumbufu.

***vii. Kuimarisha michezo kwa makundi maalumu ya Wanawake na Walemavu***

Katika eneo hili Wajumbe waliuliza kuhusu mpango makakati wa maendeleo ya michezo na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu na wanawake.

a. Wajumbe walitaka kufahamu kama wanamichezo wanawake na wenye ulemavau kutoka Zanzibar wameshirikishwa katika mpango huo. Maelezo ya majibu ya hoja hizo ni kuwa mpango huo mkakati umezinduliwa mwezi Septemba 2021 umehusisha maeneo yote muhimu kuanzia wataalamu, vifaa na fedha. Serikali imelipa fedha kwa timu ya walemavu kushiriki mashindano ya Olimpiki ya Walemavu yaliyofanyika jijini Tokyo Japan, vilevile imelipa gharama za usafiri kwa timu za mpira wa miguu ya walemavu yaliyofanyika Nairobi. Mpango huo umeshirikisha makundi mengine ya wanawake na walemavu. Mfuko huo umepitishwa na Bunge kiasi cha shilingi bilioni 1.5 sambamba na fedha nyengine zitakazopatikana katika mfuko wa bahati nasibu.

b. Kuimarishwa stahiki za walimu wanaofundisha watu wenye ulemavu na kupatiwa motisha wa kazi. Wajumbe walishauri kuwa walimu hawa watazamwe stahiki zao kwa kuwa kazi wanayofanya

ni ngumu sana. Shauri hili limepokelewa na Serikaili kufanyiwa kazi.

***viii. Elimu na Ajira kupitia Lugha ya Kiswahili;***

Katika eneo hili wajumbe walisisitiza umuhimu wa kukifanya Kiswahili kuwa na tija. Wajumbe wameshauri kuwa Serikali itumie Mabalozi wa Tanzania waliopo nchi za nje kukitangaza Kiswahili na kutafuta fursa za ajira kwa walimu walipo Tanzania. Ushauri huu umepokelewa na utafanyiwa kazi katika mipango ya kukuza lugha ya Kiswahili na kuleta tija kwa wananchi.

**0.5 MAONI NA MAPENDEKEZO YA WAJUMBE**

i. Wananchi waendelee kuelimishwa faida za Muungano; kwakuwa Muungano umeendelea kuwa kilelezo cha umoja, mshikamano na udugu kwa wananchi wa pande zote mbili.

ii. Wananchi wapatiwe uwelewa kuhusu utatuzi wa changamoto za Muungano; kuna umuhimu mkubwa pale changamoto za muungano zinapopatiwa ufumbuzi wananchi wafahamishwe kwa kina namna ya utekelezaji wa makubaliano hayo.

iii. Uwepo Mkakati maalumu wa kisheria wa kudumisha na kuendeleza Mashirikiano ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

iv. Uwepo ufuatiaji wa Karibu wa utekelezaji wa mambo yaliyokubaliwa na kupatiwa ufumbuzi

v. Baraza la Wawakilishi litekeleze kikamilifu masharti ya Kanuni ya 137 (5) ambayo inaelekeza Baraza kutoa azimio maalumu kwa Wajumbe wa Baraza wanaowakilisha Bungeni kwa ajili ya kuwasilisha maoni yao.

vi. Utaratibu wa kikatiba wa kuliwakilisha Baraza la Wawakilishi Bungeni uwe endelevu kama wasisi wetu wa Mapinduzi, Muungano na Bunge la Jamhuri walivyoanza na kuendeleza hadi sasa.

vii. Sekretarieti ya Wabunge watano kutoka Barazani iendelee kuimarishwa ili iweze kufanya kazi zake kwa wepesi.

## 0.6 HITIMISHO

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waendelee kuwaamini, kuwa karibu nao na kuendelea kutoa mashirikiano kwa Wajumbe wanaowakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa kuwa kazi inayofanyika kule ni kwa niaba yao.

Nachukuwa nafasi hii kwa upekee kuwapongeza viongozi wetu wakuu wa nchi yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mashirikiano yao makubwa na uongozi wao mwema ambao umeiweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu na kasi ya maendeleo tunayoishuhudia kila siku na kudumisha Muungano wetu ambao unazidi kuwa imara. Tunawapongeza sana.

Mwisho kabisa, nitowe shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na wasaidizi wake wote kwa kutuongoza vyema katika Baraza letu la Wawakilishi na kutusimamia katika shughuli zetu mbalimbali.

Nawashukuru Wajumbe **WOTE** wa Baraza la Wawakilishi kwa imani yao kubwa kwetu kwa kutuchagua kwenda kuwawakilisha Bungeni, na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wote tunawashukuru kwa mashirikiano yao, maoni na ushauri wanaotupatia kwa nyakati tofauti kwa ajili ya kutimiza majukumu waliyotutuma.

Lakini nisisahau, kwa niaba ya wenzangu, kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Msellem kwa kutupatia usaidizi wa kutosha kuratibu na kuandaa ripoti hii. Kwa kipindi kirefu Wabunge wa Baraza hawakuwa na Sekeretarieti ya kuratibu kazi zao na kuandaa ripoti, nadhani pia hili limechangia Wajumbe hawa kushindwa

kuwasilisha taarifa zao hapa Barazani, tunamshukuru Katibu wa Baraza na timu yake kwa ubunifu wao ambao umetupa wepesi wa kufanya kazi zetu.

Nitowe shukurani za dhati kwa chama chetu cha Mapinduzi (CCM) na viongozi wetu, Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Mwenyekiti wetu wa *Caucus*, Mnadhimu wetu, na viongozi wengine wote wa chama kwa miongozo yao na kwa pamoja tunaahidi tutaendelea kutoa ushirikiano katika nafasi zetu kuhakiksha tunatekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ili wananchi wetu waendelee kuwa na imani na kuendelea kuichagua CCM katika uchaguzi mkuu wa 2025.

Mwisho kabisa lakini siyo kwa umuhimu nawashukuru sana Wajumbe wenzangu wote tunaowakilisha Baraza la Wawakilishi Bungeni kwanza kwa kunichagua kuwasilisha taarifa hii, na kwa mchango mkubwa na kazi kubwa waliyofanya katika kutayarisha taarifa hii ambayo kwa niaba yao leo hii nimeiwasilishwa mbele ya Baraza hili.

Nawashukuru kwa michango yao Bungeni, wamechangia vizuri katika maeneo mbali mbali kwa nia ya kushauri, kutoa mapendekezo na kuelekeza kama Kanuni na taratibu za Bunge zinavyoelekeza. Kwa heshima naomba niwataje kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
2. Mhe. Bakari Hamad Bakar
3. Mhe. Ameir Abdalla Ameir
4. Mhe. Bahati Khamis Kombo
5. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman

Kwa kumalizia, kwa niaba ya wenzangu wote namshukuru Katibu wetu Ndugu Khamis Hamad Haji, ambaye pia ndiye Mratibu wetu wa shughuli za Kamati Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa aliyofanya kuratibu taarifa zetu na hatimaye tumeweza kuwasilisha hapa Barazani, tunamshukuru sana.

Baada ya kueleza hayo, nawashukuru sana Wajumbe kwa kunisikiliza na nakushukuru Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

……………………..

Mwantatu Mbarak Khamis

Mjumbe Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar**